# WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

# SHULE YA SEKONDARI RUHUWIKO

**Reg. No. S.0756**

**S.L.P. 448,**
**SONGEA.**

**Simu: 0764416155/0754636049/0621064022**
**Tovuti: www.ruhuwikoschools.ac.tz**
**Barua pepe: ruhuwikosecschool@gmail.com**

**Tarehe: ………………………**

**JINA LA MWANAFUNZI: …………………………………………………………………………………………………………….**

## YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS) KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO 2021 / 2022

**1.0. UTANGULIZI**

Napenda kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Ruhuwiko Kidato cha **TANO** Mwaka 2021/2022. **Shule itafunguliwa tarehe 05/07/2021**. Kutakuwa na masomo ya awali (Pre Form Five) kwa wanafunzi wenye sifa za kujiunga na kidato cha tano ambao watapenda kuanza mapema kabla ya muda wa kufungua shule rasmi. Masomo hayo yameshaanza na yanachangiwa gharama ya **Tshs. 300,000/= tu** kwa wanafunzi wa BWENI na **Tshs. 200,000/= tu** kwa wanafunzi wa KUTWA. *Gharama hizo zilipwe Benki tu.*

**1.1. MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya Sekondari Ruhuwiko ipo katika eneo la JWTZ Kikosi cha Huduma (411 KJ) katika Manispaa ya Songea barabara iendayo Mbinga.

**2.0. NAMNA YA KUJISAJILI**

Ufikapo shuleni unatakiwa kuripoti ofisi ya Usajili ukiwa na **Fomu ya Maombi**, **Picha moja** (Passport), **Cheti Cha Kumaliza Kidato Cha Nne** au **Cheti cha Matokeo ya Kidato cha Nne** ***(Result Slip)*** pamoja na nakala ya **Cheti cha Kuzaliwa**.

**3.0. MALIPO YA ADA**

| ADA YA BWENI | ADA YA KUTWA |
|---|---|
| **Julai – Septemba - Tshs. 345,000/=** | **Julai – Septemba - Tshs. 240,000/=** |
| **Oktoba – Disemba - Tshs. 345,000/=** | **Oktoba - Disemba - Tshs. 240,000/=** |
| **Januari - Machi - Tshs. 345,000/=** | **Januari - Machi - Tshs. 240,000/=** |
| **Aprili – Juni - Tshs. 345,000/=** | **Aprili – Juni - Tshs. 240,000/=** |
| **Kwa Mwaka = Tshs. 1,380,000/=** | **Kwa Mwaka = Tshs. 960,000/=** |

***ZINGATIA: ADA IKILIPWA HAITARUDISHWA***

Malipo ya ada ya shule yalipwe kupitia benki tu kwenye **A/C No. 023101000790 NBC**, **A/C No. 01J1085291000 CRDB** na **A/C No.61803500130 NMB** jina la akaunti ni **MKUU WA SHULE RUHUWIKO SEKONDARI** na "Original Pay in Slip" iletwe Shuleni Ofisi ya Ada. Kumbuka kuandika Majina ya Mwanafunzi kwenye risiti ya Benki wakati wa kulipa Ada. Hakuna malipo yoyote ya fedha taslimu yanayopokelewa shuleni, **isipokuwa fedha za sare**.

**4.0. SARE (UNIFORMS)**

Mwanafunzi **huruhusiwi** kujishonea Sare za Shule. Sare zote zinashonwa shuleni kwa gharama zifuatazo:-

**a) Wavulana**

i. Suruali mbili rangi ya bluu bahari Tsh. 35,000/=
ii. Sweta1 rangi ya bluu bahari Tsh. 17,000/=
iii. T-shirt 1 Tsh. 15,000/=
iv. Nguo ya kazi 1 (Shamba Dress) Tsh. 32,000/=
v. Tai 1 Tsh. 2,000/=

**Jumla ya Gharama za Sare**
Wavulana wa Bweni - **Tshs. 101,000/=**
Wavulana wa Kutwa - **Tshs. 69,000/=**

**b) Wasichana**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Sketi mbili rangi ya bluu bahari | Tsh. 41,000/= |
| ii. | Sweta1 rangi ya bluu bahari | Tsh. 17,000/= |
| iii. | T-shirt | Tsh. 15,000/= |
| iv. | Nguo ya kazi 1 (shamba dress) | Tsh. 26,000/= |
| v. | Tai 1 | Tsh. 2,000/= |

**Jumla ya Gharama za Sare**

Wasichana wa Bweni - **Tshs. 101,000/=**

Wasichana wa Kutwa - **Tshs. 75,000/=**

**c) Mzazi/mlezi mnunulie mwanao:-**

i. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi
ii. Viatu vyeusi vya Kamba
iii. Soksi nyeusi na mkanda mweusi kwa wavulana na soksi nyeupe kwa wasichana

## 5.0. HUDUMA YA AFYA

Shule haigharamii matibabu ya Mwanafunzi. Kila Mwanafunzi anatakiwa kuja na **Bima ya Afya** na kwa wale ambao hawana wanatakiwa kuja na **Fedha Taslimu (Cash) Tshs. 50,400/=** kwa ajili ya kukatiwa bima ya Afya.

## 6.0. VIFAA VYA DARASANI NA MAZINGIRA

a. Kamusi kubwa (English – English Oxford Dictionary)
b. Daftari kubwa (*Counter Books*) – idadi kulingana na masomo unayosoma.
c. Vitabu vya Masomo **(Orodha ya Vitabu Imeambatanishwa na ni Muhimu kuwa navyo).**
d. Karatasi za kurudufu (Ream $A_4$) bunda moja kila muhula.
e. Fagio la mpira la kudekia – mopa (*Rubber squeeze*) –1.
f. Ndoo moja ya plastiki ya lita 20, Ufagio wa Chelewa -1.
g. Jembe moja lenye mpini, Fyekeo/kwanja 1.
h. Brashi ngumu fupi 1 na Fagio laini ndefu 1.
i. Kila mwanafunzi awe na Saa ya mkononi na Leso nyeupe.

## 7.0. VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI WA BWENI

a. Nguo za Michezo *(**tracksuit rangi ya bluu iliyokolea**)*, pamoja na viatu vya michezo *(raba).*
b. Godoro la futi $2^1/_2$, Shuka mbili rangi ya **Bluu iliyokolea**, Blanketi 1, mto na Chandarua (net).
c. Sanduku imara la chuma (Tranka) na Kufuli imara.
d. Taulo, Kandambili na Ndoo ya lita 10 ya kuogea.
e. Vyombo vya kulia Chakula.
f. Kanga mbili kwa wasichana.
g. Vitu vidogovidogo kwa matumizi yake binafsi.

## 8.0. NGUO MAALUMU ZA KUVAA BAADA YA VIPINDI (SHAMBA DRESS)

Wanafunzi bweni wanavaa nguo za kazi baada ya muda wa masomo na siku zote ambazo sio za masomo *(weekend days)*. Utaratibu huu ni **wa lazima** kwa kila mwanafunzi wa bweni ili kudumisha nidhamu, kuondoa vishawishi vya wizi wa mavazi ya nyumbani na tabia nyingine mbaya zinazoambatana na uvaaji wa nguo za nyumbani. Mvulana atashonewa na shule shati na suruali jozi moja na msichana atashonewa na shule gauni la heshima (refu). **Nguo za nyumbani haziruhusiwi** na ukaguzi unafanywa mara mwanafunzi anapofika Shuleni.

## 9.0. MAMBO MENGINE YA KUZINGATIA:

i. **Wastani wa Shule**:- Mwanafunzi anatakiwa kupata wastani wa kuanzia **60%** na kuendelea katika masomo yake yote ili awe amefaulu mitihani ya ndani na kuendelea na Kidato cha Sita.
ii. **Simu haziruhusiwi kabisa kwa Wanafunzi**: Mwanafunzi atakayekamatwa na simu hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuchoma simu na mwanafunzi kusimamishwa Shule mara moja.
iii. **Sheria za shule:-** Kila mwanafunzi atapewa nakala ya Sheria za Shule ambazo anatakiwa kuzifuata kikamilifu.

**KARIBU SHULE YA SEKONDARI RUHUWIKO UPATE ELIMU BORA NA NIDHAMU THABITI.**

……………………

**MKUU WA SHULE**